

Siku ya Kimataifa ya Hewa Safi kwa anga za bluu ya 2020



Siku ya Kimataifa
ya Hewa Safi ili kuwa
na mawingu ya bluu



#HewaSafiKwaWote

Siku ya Kimataifa ya Hewa Safi kwa anga za bluu ya 2020


Mnamo Septemba 7, 2020, kwa mara ya kwanza dunia itasherehekea Siku ya Kimataifa ya Hewa Safi kwa anga za bluu—na kuuchochea ulimwengu kuchukua hatua ya kupambana na uchafuzi wa hewa, mojawapo kati ya changamoto kubwa zaidi za kiafya na kimazingira za wakati wetu. Siku hiyo inatualika sote kuzingatia jinsi tunavyoweza kutegemeza hatua zinazochangia kuwepo kwa hewa safi katika nchi zetu, miji na biashara, na kufanya mabadiliko katika maisha yetu ya kila siku ili kupunguza uchafuzi wa hewa. Kadhalika, vitendo hivyo, hufaidi afya za watu na kupunguza uchafuzi unaoongeza joto la hewa na gesi ya nyumba ya kioo.



www.cleanairblueskies.org

Uchafuzi wa hewa ni nini na kwa nini ni muhimu kwangu?

Watu tisa kati ya 10 ulimwenguni wanapumua hewa chafu. Uchafuzi wa hewa ndilo suala muhimu zaidi la kiafya la wakati wetu, linalosababisha kifo 1 kati ya 9 ulimwenguni kote na wastani wa vifo milioni 7 vya mapema kila mwaka. Uchafuzi wa hewa husababisha kifo kutokana na maradhi ya moyo, magonjwa ya mapafu, saratani ya mapafu na kiharusi. Kadhalika, uchafuzi wa hewa huumiza mazingira yetu ya asili, hupunguza usambazaji wa oksijeni katika bahari zetu, na kufanya iwe vigumu kwa mimea kukua na kuchangia mabadiliko ya hali ya hewa. Lakini uchafuzi wa hewa unaweza kuzuiwa. Hatua za kusuluhisha zinajulikana na zinaweza kutekelezwa. Ulimwengu unahitaji **kuchukua hatua sasa.**



Ni nini vyanzo tofauti vya uchafuzi wa hewa?

Shughuli tano za wanadamu ndizo chanzo kikuu cha uchafuzi wa hewa. Sera na utendakazi bora unaweza kupunguza kwa kiasi kikubwa uchafuzi kutoka kwa kila sekta



1. Kilimo


Methani, inayozalishwa kupitia mbinu za kilimo na mifugo, inachangia kiwango cha chini cha ozoni, na kusababisha pumu na magonjwa mengine ya kupumua. Pia ni gesi ya nyumba ya kioo yenye nguvu inayochangia kuongezeka kwa joto duniani. Kuwasha moto katika eneo ili kusafisha mashamba na ardhi kunachangia kwa kiasi kikubwa zaidi kaboni nyeusi na uchafuzi wa chembechembe ndogondogo.

www.cleanairblueskies.org



2. Usafiri

Chembechembe ndogondogo, ozoni, kaboni nyeusi na nitrojeni dioksaidi vyote vimehusianishwa na uchafuzi kutoka kwa sekta ya usafiri duniani. Uchafuzi wa gari husababisha vifo vya mapema 400,000 kwa mwaka na hugarimu takriban trilioni \$1 katika uharibifu wa afya.



3. Nyumbani

Chembechembe ndogondogo, kaboni monoksaidi, madini ya risasi na zebaki ndivyo vyanzo vikuu vya uchafuzi unaotokana na kuchoma fueli manga katika moto wazi na majiko yasiyofaa ndani ya nyumba. Uchafuzi wa hewa nyumbani husababisha vifo vya mapema kwa watoto wachanga milioni 4.3 kila mwaka.



4. Viwanda

Kiasi kikubwa cha kaboni monoksaidi, haidrokaboni, chembechembe ndogondogo na kemikali huruhusiwa na viwanda kuingia hewani.



5. Taka

Methani, chembechembe ndogondogo na sumu nyingine zote hutolewa kupitia uchomaji wa taka. Kuchoma taka katika maeneo yaliyo wazi pia hutokeza uchafuzi unaodumu wa kemikali za sumu za kikaboni ambazo huingia kwenye mkondo wa chakula.

Tazama [hapa](#) kwa taarifa zaidi kuhusu vyanzo na athari za uchafuzi wa hewa

Kwa nini uchafuzi wa hewa ni suala la dharura sasa?

-Afya

Ushahidi wa athari ya uchafuzi wa hewa kwa afya ya binadamu ni wazi na inaongezeka. Umehusianishwa tangu jadi na ugonjwa wa moyo na mishipa na ya kupumua, katika miaka ya hivi karibuni mfiduo kwa uchafuzi wa hewa umegunduliwa kutatiza anuwai ya mifumo ya kibaolojia na maendeleo ikiongeza hatariza ugonjwa wa sukari, ugonjwa wa kupoteza kumbukumbu, tatizo la ukuzi wa akili na viwango vya chini vya kufikiri. Karibu watu milioni 7 ulimwenguni hufa mapema kutokana na uchafuzi wa hewa kila mwaka.

- Haki za Kibinadamu

Katika angalau mataifa 155, mazingira yenye afya hutambuliwa kama haki ya kikatiba. Majukumu yanayohusiana na hewa safi yamewekwa katika vyombo kadhaa vya haki za kibinadamu vya kimataifa, kutia ndani Universal

Tangazo la Haki za Kibinadamu na Makubaliano ya Kimataifa Kuhusu Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kitamaduni.

- Hewa Safi na Malengo ya Maendeleo Endelevu

Kutimiza haki ya kupumua hewa safi kunaenda sambamba na kufanikisha Maendeleo Endelevu Malengo, kutia ndani maisha yenye afya kwa wote, miji endelevu, uwezo wa kupata nishati safi duniani kote na hatua madhubuti za kushughulikia mabadiliko ya hali ya hewa.

- Hali ya hewa

Uchafuzi wa hewa na mabadiliko ya hali ya hewa zinahusiana sana kwa kuwa zinashiriki vyanzo sawa. Kwa hivyo hatua za kudhibiti zilizoandaliwa vizuri zinaweza kupata mafanikio katika hali ya hewa na ubora wa hewa ya eneo hususa. Kwa mfano, vipimo kumi na sita vya kudhibiti uchafuzi wa mazingira wa muda mfupi vinavyoshughulikia vyanzo vikuu vya methani na kaboni nyeusi, vinaweza kupunguza kwa wakati huo huo joto duniani hadi 0.5°C kwa

miongo michache ijayo, kuepusha vifo vya mapema vya watoto wachanga milioni 2.4 vinavyotokana na uchafuzi wa hewa na kuepusha upotezaji wa mazao zaidi ya tani milioni 50 kwa mwaka kutokana na ozoni sehemu ya chini ya anga.

- Mazingira

Uchafuzi wa hewa huathiri mazingira. Unaweza kubadilisha au kumaliza virutubisho katika ardhi na njia za maji, kuhatarisha vyanzo muhimu vya maji safi, kuumiza misitu na kupunguza mavuno ya mazao, kutokeza sumu na vyuma vizito kwenye mnyororo wa chakula na kuharibu taswira za kitamaduni kama vile minara ya ukumbusho na sanamu.

- Uchumi

Athari dhahiri za kiuchumi za uchafuzi wa hewa ni gharama kwa afya ya umma. Uchafuzi wa hewa hugarimu uchumi wa dunia zaidi ya US\$5 trilioni kila mwaka katika gharama za ustawi. Athari hizo ni mbaya zaidi katika ulimwengu unaostawi, ambapo katika maeneo fulani, upotezaji wa ustawi umegharimu karibu asilimia 7.5 ya Pato la Taifa (GDP).

Pamoja tunaweza kufanikisha #HewaSafiKwaWote

Kila mtu anaalikwa kushiriki! Chunguza wavuti wa Siku ya Kimataifa ya Hewa safi kwa anga za bluu ili ujifunze kuhusu aina mbalimbali za uchafuzi wa hewa na kwa nini ni muhimu kwako kwa kutumia picha zenye ujumbe, majaribio na hadithi kutoka ulimwenguni pote.

Serikali, majiji, shule, biashara, mashirika:

- Tumia wavuti wa Siku ya Kimataifa ya Hewa safi kwa anga za bluu na mwongozo huu unaotumika ili kupata kichocheo kuhusiana na aina za shughuli unazoweza kuwajibikia mnamo Septemba 7 na kuandikisha hafla zako kwenye wavuti. Hizi zinaweza kuhusisha kufanyia kazi nyumbani, kuendesha baiskeli unapoenda kununua mboga au kuhamasisha jiji lako kuanzisha siku ya kutotumia gari.

- Hafla zote zilizosajiliwa zitaonyeshwa ulimwenguni kwenye wavuti kupitia ramani halisi.
- Katika majuma yanayofuata Siku ya Kimataifa ya Hewa safi kwa anga za bluu, wavuti huu utashiriki hadithi juu ya ahadi zilizotolewa na miji, serikali na sekta ya kibinafsi na kufuatilia jinsi ambavyo kwa pamoja tumesogeza sindano katika uchafuzi wa hewa na tutadumisha utendaji wake kwa mwaka mzima tunapojiandaa kwa ajili ya 2021!



Serikali zinaweza vipi kuhusika?

Fikiria kutumia Siku ya Kimataifa ya Hewa Safi kwa anga za bluu kuweka wajibu wa kuongeza ubora wa hewa. Haya ni baadhi ya maoni:

- Katika kujiandaa kwa ajili ya Septemba 7, panga kampeni, hafla na shughuli za kuhamasisha jamii na ushirikishe umma kwa ujumla ili kujenga maarifa na kuongeza hatua za kupambana na uchafuzi wa hewa.
 - Jiunge na BreatheLife kuongeza uhamasishaji wa umma juu ya athari za kiafya na za hali ya hewa zinazotokana na uchafuzi wa hewa na uwajibike kufuatilia maendeleo, shiriki matukio na mazoea bora kupitia Mtandao wa BreatheLife.
 - Tekeleza viwango vya pamoja vya ubora wa hewa na sera zilizotengenezwa za mabadiliko ya hali ya hewa ili kufanikisha kwa wakati huo huo maadili ya Mwongozo wa Ubona wa Hewa ya WHO
- na wajibu wa hali ya hewa wa Mkataba wa Paris.
 - Wajibika Kutathmini idadi ya maisha yanayookolewa, faida za kiafya kwa watoto na vikundi vingine vilivyo hatarini, na gharama za kifedha kwa mifumo ya afya zinazoepukwa zinazotokana na kutekelezwa kwa sera mpya.
 - Tekeleza sera za uhamaji kielektroniki na uhamaji endelevu na hatua zenye lengo la kufanya maamuzi thabiti yatakayoathiri uchafuzi unaotokana na usafiri wa barabarani.
 - Tangaza masharti mapya ya kupunguza vyanzo hatari vya uchafuzi wa hewa vinavyotoka viwandani.
 - Wajibika kuondoa magari yanayotumia petroli na dizeli.
 - Ahidi kuwekeza zaidi katika vyanzo vya nishati vinavyoweza kutumiwa tena.
 - Weka sera zinazoongeza uwezo wa kupata vyanzo vya nishati safi, visivyochafua hewa katika nyumba zote.
- Shikamana na sera zinazoboresha usimamizi kamili wa taka katika manispaa na kupunguza uchafuzi unaotokana na sekta hiyo.
 - Ahidi kupunguza kiasi cha pesa zinazotoka kwa mafuta ya kisukuku.
 - Wajibika kuunganisha ubora wa hewa na upangaji wa hali ya hewa, usimamizi na takwimu za uchafuzi.
 - Wajibika kuchunguza ubora wa hewa, tathmini vyanzo vya uchafuzi na kukabiliana navyo ili kuwalinda raia kutokana na sumu hatari.
 - Wajibika kutekeleza mikakati ya mipango ya hali ya hewa ya maeneo ya karibu na ya kitaifa.
 - Wajibika kufanya kazi kuelekea na kutetea hatua za kikanda, kitaifa na kimataifa kuhusiana na vyanzo vilivyo nje ya mipaka yako.

Lisajili tukio lako [hapa](#)

Majiji yanaweza kusherehekea vipi?

Fikiria kutumia Siku ya Kimataifa ya Hewa Safi kwa anga za bluu kuhamasisha watu kuhusu hatua ambazo mji wako unachukua kuboresha ubora wa hewa. Haya ni baadhi ya maoni:

- Andaa usafiri wa umma bila malipo katika maeneo ya mijini ili kuwatia moyo madereva kuacha magari yao nyumbani.

- Panga matembezi katika maeneo yenye mazingira ya asili na hafla za kuendesha baiskeli kwa ajili ya umma ili kuwatia watu moyo kutembea na kuendesha baiskeli.
- Panga shughuli za upandaji miti.
- Jenga barabara zisizoruhusu magari.
- Wajibika kupanua nafasi zenye mimea mijini.
- Panga tukio la ana kwa ana au la mtandao na maofisa wa jiji na wataalamu wa afya.

- Fanya kazi na wasanii na wanamuziki katika kupanga hafla na maonyesho yanayohamasisha watu katika jiji lako.
- Shiriki vifaa vya kufundishia mtandaoni kwa ajili ya shule za mitaa.
- Shiriki picha, video na hadithi kwenye mitandao ya kijamii kwa kutumia #HewaSafikwaWote.

Lisajili tukio lako [hapa](#)



Biashara zinaweza kuhusika kiviipi?

Tumia Siku ya Kimataifa ya Hewa Safi kwa anga za bluu kuweka ahadi za kupunguza uchafuzi na kuwekeza katika utafiti na maendeleo ili kuwazia njia mpya na zisizo na uharibifu za kufanya biashara.

- Weka ahadi ya kutumia vifaa vinavyoweza kutumiwa tena kwa bidhaa zako na kupunguza na hatimaye kuondoa taka kutoka katika mzunguko wa biashara yako.
- Hakikisha chanzo cha nishati yako kinaweza kutumiwa tena.
- Jaribu kupitisha hewa safi ili kupunguza joto au weka mifumo ya haidroflorokaboni inayofanya kazi vizuri sana ili kupunguza joto.
- Ahidi kununua magari yanayotoa uchafu mdogo au yanayotumia umeme kwa ajili ya kampuni.
- Fikiria jinsi unavyoweza kupunguza uchafuzi wa hewa unaotokana na vituo na mikondo ya usambazaji.

Lisajili tukio lako [hapa](#)



Asasi za kiraia zinaweza vipi kushiriki?

Katika Siku ya Kimataifa ya Hewa Safi kwa anga za bluu, sisi sote tunapaswa kufikiria kuhusu kuweka ahadi za kuendelea zaidi kutumia na kupunguza uchafuzi wa hewa katika maisha yetu ya kila siku. Haya ni baadhi ya madokezo ya kuanzia:

- Wajibika kukuza na kutumia usafiri wa umma zaidi, kuendesha baiskeli au kutembea mwendo mfupi, na kushiriki gari moja na wengine inapowezekana.
- Wajibika kupunguza na kutumia tena taka.
- Panga shughuli ya kupanda miti.
- Panga hafla ya kuondoa taka.
- Fikiria jinsi ambavyo kupambana na uchafuzi wa hewa kunaweza kuratibiwa kati ya shughuli zako.

- Panga hafla za umma na kampeni za kuboresha maarifa ya umma na hatua za kushughulikia suala la uchafuzi wa hewa.
- Tetea na uunge mkono mamlaka ya umma katika utekelezaji wa mipango ya kushughulikia suala la uchafuzi wa hewa
- Fanya kazi na wasanii na wanamuziki katika kupanga hafla na maonyesho yanayokuza uhamasishaji katika jamii zenu.
- Tumia Siku ya Kimataifa ya Hewa Safi kwa anga za bluu kama fursa ya kuwaomba viongozi wa maeneo yenu kutoa taarifa kuhusu ubora wa hewa kwa wakati unaofaa, na kwa ukawaida na kuomba kuwe na sheria zinazowadhibiti wachafuzi wabaya zaidi.

Lisajili tukio lako [hapa](#)



Shule na vyuo vikuu vinaweza vipi kusherehekea?

Siku ya Kimataifa ya Hewa Safi kwa anga za bluu inaweza kuwa jukwaa la wanafunzi na maafisa wa elimu kuongoza mapambano kwa ajili ya hewa safi na kuomba serikali zao na shule kuanza kutumia nishati safi zaidi. Hii ni baadhi ya mifano ya hatua zinazoweza kuchukuliwa na shule na vyuo vikuu:

- Ikiwa shule na vyuo vikuu vimefunguliwa au vitafunguliwa, waombe wanafunzi walete miche kwa ajili ya hafla ya upanzi wa miti.
- Chunguza chaguzi na utangaze
- katika Siku ya kuweka vipimo vya kuchunguza ubora wa hewa ili jamii ifahamu hewa wanayopumua.
- Waombe walimu na maprofesa wafundishe kuhusu uendelevu na ubora wa hewa.

- Wajibika kuandaa mabasi ya umeme na kufanya uendeshaji wa baiskeli kufurahiwa katika shule yako.
- Wasaidie wanafunzi kuanzisha vilabu vya mazingira, mtandaoni au kwenye vyuo vikuu, vinavyoweza kuwapa vijana uwezo wa kuwa wabunifu na kupata maoni ya kukabiliana na uchafuzi wa hewa.
- Gundua na uwajibike katika Siku kuhusiana na kutumia nishati mbadala kwenye vyuo vikuu.
- Tenga sehemu zisizoruhusiwa magari karibu na shule yako au vyuo vikuu.
- Husisha sehemu za masomo na shughuli ili kuboresha maarifa ya wanafunzi na hatua zinazohusiana na masuala ya mazingira kwa ujumla na khususa kuhusu kupunguza uchafuzi wa mazingira.

Lisajili tukio lako [hapa](#)




Ni vipi watu wanavyoweza kuhusika?

Watu tisa kati ya kumi wanapumua hewa iliyochafuliwa. Kuanzia 23 Agosti, hadi Siku ya Kimataifa ya Hewa Safi kwa anga za bluu mnamo Septemba 7, tunatoa wito kwa kila mtu kuhamasisha #HewaSafiKwaWote . Pamoja na watu mashuhuri, washawishi na waundaji, hii Siku ya Kimataifa ya Hewa Safi ya anga za bluu, kila mmoja anaalikwa kuzingatia, kuwajibika na kutangazia familia, marafiki, marika na miungano mikubwa zaidi kwenye mitandao ya kijamii:

- Tumia usafiri wa umma, endesha baiskeli au tembea ili kufika sehemu fulani.
- Punguza kiasi chako cha taka, chakula cha mbolea, takataka zisizo za kikaboni, tumia tena mifuko ya mboga na usichome takataka.

- Badilisha lishe na uanze kula milo inayotokana na mimea, punguza sana matumizi ya bidhaa za plastiki zinazoweza kutumiwa mara moja tu, na ufikirie kutumia usafiri ulio na uchafuzi mdogo.
- Hifadhi nishati, zima taa na vifaa vya umeme wakati havitumiki.
- Angalia makadirio ya ufanisi wa mifumo ya kupasha nyumba joto na jiko ili kutumia mifumo inayookoa pesa na kulinda afya.
- Kuanzia Agosti 23 hadi Septemba 6, chapisha kwenye mitandao ya kijamii hatua ambazo wewe mwenyewe utachukua ili kupunguza uchafuzi wa hewa na uwahusishe katika chapisho hilo watu 3 / mashirika / kampuni zilizo na alama ya reli **#HewaSafiKwaWote**.
- Mnamo Septemba 7, wakati Siku ya Kimataifa ya Hewa Safi ya anga za bluu itaadhimishwaulimwenguni kote, fanya chapisho jingine katika mtandao wa kijamii kwa kuchukua picha au video yako mwenyewe ukitimiza wajibu wako na utumie alama ya reli **#HewaSafiKwaWote**.

www.cleanairblueskies.org





**Siku ya Kimataifa
ya Hewa Safi ili kuwa
na mawingu ya bluu**

**Isajili hafla yako au shughuli kwa Siku ya Hewa
Safi ya anga za bluu ya kwanza**

www.cleanairblueskies.org